CHANJO YA PEPOPUNDA (TETANUS TOXOID)

21 AGOSTI 2009

KABELWA KAGARUKI

AINA ZA KINGA-UGONJWA

i) Kinga ya asili – mtu huzaliwa nayo (Natural immunity).

ii) Kinga ambayo mwili hutengeza baada ya viini kuingia mwilini (Artificial immunity).

- Kinga-ugonjwa ya aina moja huzuia aina moja tu ya ugonjwa

Kinga Ugonjwa (Immunity)

- Viini vya ugonjwa viingiapo mwilini, mwili hujaribu kuvipanga viini hivyo au sumu yao kwa kutengeneza kinga-mwili (anti-bodies)
- Wakati mwingine mwili peke yake hauwezi kutengeneza kinga-mwili ya kutosha kupigana na viini vya ugonjwa kwa hiyo mtoto akiambukizwa huugua
- Mtoto akipewa chanjo zinamsaidia kutengeza kinga-mwili kwa ugonjwa

CHANJO (VACCINES)

- Chanjo hutengenezwa kitaalaM ili zizuie magonjwa
- Hutengenezwa kutokana na viini vinavyosababisha ugonjwa husika
- Hutolewa kwa njia mbali mbali k.v. sindano, matone ya mdomoni
- Chanjo hizi hazitibu magonjwa bali zinakinga
- Kuinga-mwili husaidia kuua viini vya ugonjwa wa aina ya chanjo aliyopewa au kuharibu sumu yao.

MAGONJWA TUNAYOZUIA KWA CHANJO

- Kifua Kikuu (Tubercullosis)
- Dondakoo (Pertussis)
- Kifaduro (Diphtheria)
- Pepopunda (Tetanus)
- Surua (Measles)
- Polio (Poliomyelitis)
- Homa ya Ini (Hepatitis type B)
- Homa ya uti wa mgongo (meningitis)
- Kichomi (Pneumonia)

CHANJO ZILIZOPO KLINIKI

- BCG – chanjo moja
- DTP-HepB-hib - chanjo tatu
- OPV – chanjo nne
- MEASLES – chanjo moja
- TT – chanjo 2 hadi tano.

CHANJO YA PEPOPUNDA (TT)

- Hutengenezwa kutokana na sumu ya viini vya ugonjwa wa pepopunda viitwavyo ***"clostridium tetani"***
- Chanjo ya TT hutoa kinga yenye nguvu sana kuzuia sumu ya viini vya ugonjwa
- Chanjo ni salama, imara
- Bei yake ni ndogo kuliko zote
- Haina madhara kwa ujauzito

CHANJO YA PEPOPUNDA (TT)

- Hutolewa kwa mwanamke yeyote mwenye umri wa kuzaa (miaka 15 hadi 49)
- Umkinga mama mjamzito na mtoto atayemzaa
- Kinga utengenezwa ndani ya mwili wa mama kisha huingia katika mwili wa mtoto
- Mtoto uzaliwa akiwa na kinga-ugonjwa ya muda mfupi
- Huweza kutolewa kwa mtu yeyote aliyepata jeraha

CHANJO YA PEPOPUNDA (TT)

- Chanjo ya TT hutolewa kwa njia ya sindano ndani ya msuli kwenye sehemu ya juu ya mkono (begani)

- Hutolewa kwa kiasi cha ujazo wa nusu mililita (0.5 ml)

RATIBA YA TT

- Chanjo ya kwanza hutolewa wakati wowote. Chanjo hii haitoi kinga mwilini
- Chanjo ya pili hutolewa baada ya wiki nne. Kinga yake ni miaka mitatu
- Chanjo ya tatu hutolewa miezi sita baada ya chanjo ya pili. Kinga ni miaka mitano.
- Chanjo ya nne hutolewa baada ya mwaka. Kinga ni miaka kumi
- Chanjo ya tano hutolewa baada ya mwaka mmoja. Kinga ni miaka ishirini (20)

RATIBA YA TT

- Ikithibitika kuwa mwanamke aliwahi kupata chanjo za pepopunda, chanjo hizo zitachunguzwa.

- Chanjo ambazo zilitolewa kwa mpangilio ulio sahihi zitahesabika na tarehe zake zitaandikwa kwenye kadi. Kisha ataendelea na chanjo zinazofuata.

AHSANTENI SANA

Contacts:-

- ruge2002@yahoo.com - 0713514616
- amwaikemwa@yahoo.co.uk- 0756 775085
- dpmanyanga@yahoo.co.uk – 0713 666676
- dmujuni@epi-moh.go.tz
- mkasakitambi@yahoo.com – 0754 222269
- fatumamganga@yahoo.co.uk- 0766643266
- cnhamza@hotmail.com - 0713402750
- kabelwakagaruki@yahoo.com - 0755072212
- nyanzala20002000@yahoo.co.uk- 0784603199